# MAONO HAYA MAKUBWA



INAVYYOMAANISHA KUTOA MACHO YAKO KWENYE UKAWAIDA NA KUYAKAZA KWENYE MAONO

**Pastor James Kalekwa**

# MAONO HAYA MAKUBWA.

INAVYOMAANISHA KUTOA MACHO YAKO KWENYE UKAWAIDA NA KUYAKAZA KWENYE MAONO.

James Kalekwa

**Orodha ya Yaliyomo**

Tabaruku .......................................................................... 4

Salamu na Utangulizi .......................................................... 5

SURA YA KWANZA: YANAYOWAENDESHA WANADAMU .................................................................... 7

SURA YA PILI: MAANA YA MAONO ...13

SURA YA TATU: MADARAJA YA MAONO: ..17

SURA YA NNE: YALIYOMO NDANI YA MAONO .........................................................................21

Kuhusu Mwandishi: ..............................................................32

Kuhusu New Vine Church: ...................................................32

Mawasiliano na Mwandishi: ..................................................33

# Tabaruku

Mfululizo wa vitabu hivi vya kieltroniki (e-books) bure kwa kila atakaye; ni himizo la kiungu ndani yangu kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari.

Ninatabaruku kitabu hiki kwa kanisa la Kristo na kwa nchi yangu niipendayo, Tanzania.

Kanisa litashinda na kushamiri zaidi!

Tanzania, ninakupenda kwa moyo wote!

## Salamu na Utangulizi

Mfululizo huu wa vitabu vya kieletroniki ni maono ambayo Mungu ameweka ndani ya mtumishi wake, mume wangu mpenzi, kama namna yake ya kuonyesha shukurani kwa Mungu kwa zawadi ya maisha.

Ninamfahamu mume wangu kama mtu anayempenda Mungu kupitiliza. Yuko tayari kulipia gharama yoyote ile kuonyesha hilo. Ni mtu anayewapenda watu wa Mungu kwa namna ambayo sijawahi kuona. Yamekuwa ni maombi yake kuyagusa maisha ya wengi kwa kadiri inavyowezekana kabla Yesu Kristo hajarudi.

Anapoadhimisha siku ya kuzaliwa kwake, amekuandikia kitabu hiki, akapangilia na kufanya kipatikane kwako bila malipo yoyote. Nimemwona anvyokesha; wakati mwingine kuamka alfajiri sana au kuchelewa sana kulala ili kukamilisha uandishi. Nimemuona anavyoomba na kuombea wasomaji, anavyojisomea na kutafiti ili kuhakikisha anafanya uwasilishaji wa thamani.

Ningependa tuthamini zawadi hii ambayo sisi wengine tunanufaika nayo bila kulipia gharama:

1. Mshukuru Mungu pamoja nasi kwa zawadi hii ya maisha ya Pastor James Kalekwa kisha muombee maisha marefu na afya njema.
2. Mwandikie ujumbe wa kumsalimu na kumpongeza ukisema ni kwa namna gani huduma

yake imeyagusa maisha yako. Ninajua hili litaufurahisha sana moyo wake.

3. Wafikishie vitabu hivi walau watu hamsini tu. Ni vitabu vinatolewa bila malipo (vimeyagharimu maisha ya mwandishi ili vikufikie).
4. Usiuze vitabu hivi. Tuligundua kuwa kuna watu wanavisambaza kwa malipo ya fedha. Hiyo si sawa. Itakuwa ni kwa hasara yako mwenyewe ukifanya hivyo.

Baada ya kuyasema hayo, nikuhakikishie ya kwamba mtu huyu mkuu wa Mungu amejaa hekima za kiungu na neno ambalo siku zote hutokeza shuhuda maishani mwa wengi. Kwa kusoma kitabu hiki, ushuhuda wako unafuatia. Nikutakie usomaji mwema.

Na heri ya kuzaliwa kwa mpendwa wetu, zawadi ya mbingu kwenye kizazi chetu, Pastor JK.

Frida James Kalekwa (Mama Pastor JK)
Mke wa mwandishi
Juni, 2024
Dodoma, Tanzania

# SURA YA KWANZA: YANAYOWAENDESHA WANADAMU

Ni vyema ukafahamu ya kwamba kwenye haya maisha kuna mambo huwaendesha watu katika kuyaendea maisha kwa ujumla na upana wake. Kinachomuendesha mtu ni msukumo, nia ya ndani, njaa au shauku. Kinachomuendesha mtu huamua apate au la; huamua ni kwa kiasi/kiwango gani apate? Huamua mwendelezo wake au kudumu kwake kwenye jambo hilo.

Nimewahi kupewa ushuhuda wa kweli na viongozi fulani kwenye kanisa moja huko kanda ya Ziwa (sitasema mkoa wala jina la kanisa kwa sababu ya maadili ya kiutumishi). Ni dada maarufu sana kwenye ulimwengu huo. Kiasi kwamba nikimtaja wengi wenu hapa mtamfahamu au mtamtafuta na kumfahamu. Aliwahi kufunga ndoa na kijana mmoja na siku kadhaa tu baada ya kufunga ndoa, aliomba kuvunja ndoa ile akiwa kwenye fungate. Akiwa na uso uliokaza na unaomaanisha. Walijaribu kuitisha vikao vya usuluhishi, lakini dada aliwaambia waendelee

na vikao kwa sababu yeye si mwanandoa tena. Alichokuwa anakitafuta amekwisha kukipata. Alitaka tu kujua ile hisia ya kuwa bibi harusi na kuvaa shera huwa inakuwaje… alitaka kujua huwa wnajisikiaje kuwa bibi harusi… na ameshajisikia tayari! Amemaliza. Ile ndoa ilidumu muda wa siku chache tu.

Ukiona watu wanatenda jambo fulani ni vyema kutaka kujua nini kinawaendesha. Hii ni pamoja na wewe... ni inahusu na mimi pia. Swali langu kubwa – Hivi mimi ninaendeshwa na nini?

Mambo kadhaa yanayoendesha watu kwenye kuyaendea mambo:

1. Maoni ya watu (Mathayo 19:12b)

*"Maana wako matowashi waliozaliwa hali hiyo toka matumboni mwa mama zao;* ***tena wako matowashi waliofanywa na watu kuwa matowashi****; tena wako matowashi waliojifanya kuwa matowashi kwa ajili ya ufalme wa mbinguni. Awezaye kulipokea neno hili, na alipokee."*

Unapendezea kuwa towashi kweli! Umekaa kitumishi! Wewe hufai kuwa na mwanamume wa namna ile! Mwanamke huyo haendani na wewe! Oroha ya maoni ya wanadamu ni ndefu… na kuna watu wanaishi, wanaamka alfajiri na mapema wakiendeshwa na maoni ya watu.

2. Maamuzi binafsi (Mathayo 19:12c)

*"Maana wako matowashi waliozaliwa hali hiyo toka matumboni mwa mama zao;* ***tena wako matowashi waliofanywa na watu kuwa matowashi****; tena wako matowashi waliojifanya kuwa matowashi kwa ajili ya ufalme wa mbinguni. Awezaye kulipokea neno hili, na alipokee."*

Ni uamuzi binafsi. Kuna kitabu kinaitwa "Kukata Maneno" kinazungumzia dhana hii ya kufanya maamuzi kwa upana. Tafuta ukisome! Sasa, kuna watu wanaendshwa na maamuzi yao ya siku kwa siku.

3. Tumbo (Wafilipi 3:19)

*"mwisho wao ni uharibifu,* ***mungu wao ni tumbo****, utukufu wao u katika fedheha yao, waniao mambo ya duniani."*

Umewahi kusikia watu wanasema ilimradi mkono uende kinywani? Watu ambao wako radhi kufanya chochote kwa ajili ya kushibisha vionjo na furaha za miili yao. Ukiwahakikishia mkate wao wa kila siku, basi hawatafanya jambo lolote aisha. Wanaishi ili wale. Duniani wamekuja kula. Hii pia imekolezwa sana na misemo ambayo kwa juu inaonekana ni hekima na kumbe kwa ndani kuna udanganyifu "Tafuta hela bwana!". Ni jambo zuri hivi. Lakini usiendeshwe… usitumikishwe… usiuze utu wako. Usiwe kama Esau.

4. Hofu (Mithali 29:25)

*"Kuwaogopa wanadamu huleta mtego; Bali amtumainiye BWANA atakuwa salama."*

Watanionaje? Watachukuliaje? Watapokeaje? Watafikirije? Hayo ni maswali yanayotokea kwenye hofu ya watu.

5. Mwenzi (Mwanzo 3:17)

"*Akamwambia Adamu, **Kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako**, ukala matunda ya mti ambao nalikuagiza,*

*nikisema, Usiyale; ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako;"*

Hii kumsikiliza mkewe haimaanishi hata kidogo kuwa na maelewano mazuri. Angalia tendo linalotendekea baada ya kumsikiliza. Kwa hiyo, ni kuelekea kwenye upotofu na uharibifu – dhambini.

6. Sifa/Umashuhuri (3 Yohana 1:9)

*"Naliliandikia kanisa neno, lakini Diotrefe,* ***apendaye kuwa wa kwanza kati yao, hatukubali.****"* 3 Yoh. 1:9

Hii ni shauku nyingine ya kutaka kuwa wa kwanza. Kutaka kuonekana mbele. Kutaka kutambulikana. Kutafuta heshima kwa nguvu.

7. Mwili (Rum 8:8/2 Pet 2:10)

*"Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu."* Warumi 8:8

*"na hasa wale waufuatao mwili katika tamaa ya mambo machafu. na kudharau mamlaka."* 2 Pet 2:10

Hii ni kuanzia vionjo na mambo yanayouvutia mwili pamoja na tabia za kimwili (carnality) ambazo zinakizanana na tabia za mtu wa ndani.

8. Ujinga (Mithali 14:17/1 Tim 1:13)

*"Yeye aonaye hasira upesi atatenda kwa ujinga;*

*Na mtu mwenye hila mbaya huzirwa."* Mithali 14:17

*"ingawa hapo kwanza nalikuwa mtukanaji, mwenye kuudhi watu, mwenye jeuri, lakini nalipata rehema kwa kuwa nalitenda hivyo kwa ujinga, na kwa kutokuwa na imani."* 1 Tim 1:13

Moja ya jambo linaloendesha wengi ni ujinga. Ile hali ya kutokujua. Kuna maamuzi mengi na hata wakati mwingine misimamo mikali ni kutokana na ujinga. Hebu fikiria ni kwa jinsi gani Mtume Paulo alaivyokuwa mchungu kwa waamini na kanisa kabla ya kuokoka… alivyoua na kudhuru kwa ujinga!

Halafu kuna kuendeshwa na MAONO sasa!

# SURA YA PILI: MAANA YA MAONO

Kupitia sura hii ni kusudio la moyo wangu ya kwamba tutajenga uelewa wa pamoja kuhusu maono kutokea kwenye msaada wa neno la Mungu na rejea kadhaa za watumishi mbalimbali wa Mungu waliowahi kufudhisha kuhusu mada hii.

Maandiko Mtakatifu yanatambulisha maono kwa kusema:

*“Pasipo maono, watu huacha kujizuia; Bali ana heri mtu yule aishikaye sheria.”* Mit 29:18 SUV

*“Pasipo maono ya kinabii watu hukosa nidhamu; heri mtu yule anayeshika sheria.”* Methali 29:18 BHN

Neno la Kiebrania linalotumika mahala pa neno la Kiswahii maono ni neno *“Chazon”* (itamke kama kha-zooni) – [matamko, unabii, mawasiliano ya kiungu]

Katika kutoa tafsiri ya neno Maono Dr. Oyedepo anasema, “Maono madhihirisho ya mpango na kusudi la Mungu kwenye maisha ya mtu. Ile kutambua KUSUDI la

Mungu kuhusiana na maisha yako ndiyo huitwa MAONO" (David Oyedepo, In Pursuit of Vision). Kwenye chapisho lake jingine anaendelea kujadili mada ya maono kwa kuongeza ya kwamba "Kujua uendako na namna gani ya kufika huko kiasi cha kujenga ujasiri wa ndani." (David Oyedepo, Understanding Vision).

Waandishi na wahudumu wengine wa injili wamezungumzia mada hii ya maono kwa mapana yake. Dr. Myles Munroe husema, "Kuona mambo ya siku za usoni/yajayo (Ni vizuri kufahamu ya kwamba Mungu anayo mawazo mazuri kwa ajili yako; anakuwazia mema; ameandika siku zako kitabuni mwake). Hata hivyo, ni vizuri zaidi kujua hayo mambo kwa umahususi wake." Anaongezea kwa kuonyesha muunganiko wa maono na kusudi la Mungu kwenye maisha ya mtu kwa kusema, "Mungu ameweka ndani ya kila mwanadamu MAONO ambayo akiyatambua huleta hali ya kusudi na maana kwenye maisha." (Dr. Myles Munroe, The Principles and Power of Vision)

Mwanamke kipofu wa macho, aliyeihudumia dunia na kuifundisha dunia maswala mbalimbali ya kiuongozi,

uandishi na hata uthubutu, Hellen Keller alisema, “Mtu fukara kuliko wote duniani ni yule asiye na maono; na mtu aliyechanganyikiwa kuliko wote ni mwenye maono lakini asiyejua namna gani ya kuyafanya yatekelezeke (yawe halisi). Na kuongeza ya kwamba “Hakuna kitu kibaya duniani kama kuwa na macho lakini hauna maono.” Hellen Keller

Kwenye kitabu chake kinachozungumzia maono, mwandishi na mkufunzi wa maswala ya uongozi na maendeleo ya mtu binafsi, Pstor Joel Nananuka anaandika na kusema: “Ni picha aliyonayo mtu juu ya maisha yake.” Kwa kukazia kuhusu kuwa na picha au taswira ya namna hiyo anajenga hojza zake kwa kusema:

- ✓ Huwezi kukiishi kile ambacho haujawahi kukiona (kwa macho ya nyama na kwa macho ya ufahamu)
- ✓ Maana ya maisha inapatikana kwenye maono. Ukikosa maono, umekosa maisha – unaweza kuwa hai lakini hauna maisha.
- ✓ Mtu mwenye maono huwa juu ya mtu mwenye rasilimali zote; mtu mwenye vipaji vyote; mwenye

> fursa zote; mwenye upako wote bila kuwa na maono (Joel Arthur Nanauka, Maono)

Kwa hiyo, kutokea hapo nimefikia kwenye hitimisho binafsi kuhusu maono ya kwamba: ni picha, muono, uelewa na kushawishika kwa ndani sasa hivi kuhusu mambo yajayo. Hutokana na Mungu. Hugusa nyanja zote za kimaisha (holistic). Yanaweza kuwa maono ya ujumla na/au maono mahususi. Mtu akiyafuata huufikia ukuu.

Kwenye sehemu zinazofuatia za kitabu nitapenda kila ukikutana na neno maono basi kichwani urejelee tafsiri hii ili tuweze kutembea kwenye mrengo na uelekeo mmoja wa kiuelewa.

# SURA YA TATU:
# MADARAJA YA MAONO:

Tunapozungumzia maono kila mtu kwa namna moja au nyingine yuko kwenye ngazi fulani kuhusu mada hii. Kuna wale ambao inawezekana hawana maono kabisa (jambo ambalo ninalisema kwa mashaka sana). Kuna kundi la wenye maono lakini hayaeleweki kwao na kwa yeyote; wengine wana maono yaliyochoka au yaliyowachosha wakati wautekelezaji; na kuna kundi la wenye maono yaliyofikia ukomo. Hebu twende tutazame na kuona kwa pamoja namna gani Bwana aweza kutusaidia hapa.

i. **Maono Mapya: (New Vision)** –

Uelekeo mpya kabisa wa kimaono. Kuna aina fulani ya maono ambayo huwa yamefungwa ndani ya muda tu. Hayana mwendelezo wa kimuda. Kwa mfano, kwenye Biblia kuna makundi kadhaa ya manabii. Namna ya kwanza ya kuwagawanya ni kwa namna waliyowasilisha unabii. Ambapo kwa mgawanyo huo utapata a). Manabii wa kuandika b). Manabii wa kunena

Halafu ukiwagawanya kwa muda na ukubwa wa kazi waliotumika ndiyo utafika mahali pa kuwa na: a). Manabii wakubwa na b). Manabii wadogo

Sasa, manabii wadogo walikuwa ni watu waliopewa unabii kwa kipindi, kundi, au ujumbe mmoja tu. Baada ya hapo kazi yao ya unabii iliisha. Kwa mfano, nabii Yona. Alikuwa ni nabii mwenye ujumbe mmoja tu; nabiikwa kundi moja tu (watu na mji wa Ninawi); na vyote vilifungwa ndani ya muda fulani mahususi. Baada ya hapo alipaswa kwenda kutafuta maono mapya!

Kuna wengine wetu upo kwenye hali ya mahangaiko kwa sababu kile unachodhani ni maono kimefikia tamati na unahita kurudi kwenye meza ya kuchorea na Mzee wa Siku upokee maono mapya.

ii. **Maono yaliyohuishwa (Renewed Vision)** –

Namna nyingine ya kufanya jambo hilo hilo; Namna iliyohuishwa ya kufanya jambo hilohilo. Ubora, vionjo za nyongeza.

Aina hii ya maono ni kubadilishiwa namna ya kufanya au njia ya kupita wakati kusudio au hitimisho linabaki kuwa

lilelile. Inawezekana ni kwa sababu ya nyakati na majira, au badiliko la makundi ya watu. Mwisho wa siku Mwenyekazi ndiye ajuaye yote.

Siku za hivi karibuni, niliwona Askofu Dr. David Oyedepo amejitokeza na kueleza ni kwa namna gani wameongeza na kuboresha namna ya uendeshaji wa huduma. Kwa hiyo, kitabu cha mwongozo cha “The Mandate” kimeboreshwa. Hivyo, aliwaalika wachungaji chini ya huduma hiyo kutafuta kitabu kipya na kuendana na maboresho hayo.

Kwa hiyo, ni jambo linalowezekana kabisa. Usiwe uliyefunga mlango kabisa kiasi kwamba Mungu akitaka kuleta uhuisho atahangaika kupata nafasi.

iii. **Maono yaliyofafanuliwa (Cleaerer Vision)** –

Hii ni maono kwa watu ambao wanaona watu kama miti wakienda. Inawezekana hapo mwanozni ulidhani umemwelewa Mungu. Lakini ulipokuja kwenye hatua za utekelezaji ulibaini ya kwamba kuna vitu havieleweki kwako.

Huu ni uhitaji wa mafafanuzi kwenye maono uliyoyakamata tayari: Ni namna ya kujibu maswali ya Nini? Nani? Wapi? Lini? Namna gani? Kwanini? kama kuondoa ukungu kwenye miwani hivi. Kwa kadiri tunavyomsogelea ndivyo inaeleweka kwa uwazi zaidi.

iv. **Maono ya kina (Deeper Vision)** –

Hapa ni hitaji la kujua kina cha maono husika. Undani wa maono. Shauku isiyoisha wala kukauka *"Nimjue Yeye; Uweza wa kufufuka kwake"* kama alivyoonyesha mtume Paulo; au alivyoimba mtunzi wa nyimbo za Kitabuni: "zaidi, zaidi... ninfahamu Yesu. Nijue Pendo lake na wokovu wake kamili."

Nimekuombea kwa Bwana ya kwamba utapokea fungu lako katika jina la Yesu. Utapokea uhuishi, ufafanuzi, na kina. Hautachanganyikiwa bali utafurahia.

# SURA YA NNE:
# YALIYOMO NDANI YA MAONO

Kwenye maono huwa kuna nini hasa? Nitarajie nini ninapoyatafuta maono haya makubwa? Nikiona nini hasa nitambue haya ni maono kutoka kwa Bwana?

1. **Mungu na uweza wake** (Isa. 6:1 - nalimwona BWANA; BWANA ni Yesu Kristo Ref: Yohana 12:41)

- ✓ Nafasi ya BWANA mst. 1
- ✓ Utakatifu wa BWANA mst. 2,3
- ✓ Uweza wa BWANA mst. 4

Maono haya kuhusu BWANA ndiyo yalimuweka Isaya kwenye amani kamilifu Ref: Isa. 26:3

*"Mungu asiyejulikana ni ngumu kutumikiwa au kuaminiwa."* A.W Pink

MDO 26:19 - Maono ya mbinguni.

MDO 26:16 - Nimekutokea; Nitakutokea.

Hivi unajua kila mara ambapo Mungu aliwatokea watu, kwa mfumo wowote ule, waliingiwa na hali ya ushangao. Ndiyo maana neno "Usiogope!" lilitumika sana. Nimekuja kwenye hitimisho ya kwamba maono makubwa ni yale ambayo yanamtambulisha Mungu na uweza wake kwa anayeona. Maono si kuhusu wewe… ukinisimulia

chochote unachokiita maono, swali langu a kwanza: Mungu yuko wapi hapo?

Kama hujamuona Mungu… tuendelee kuomba, kutafuta na kutarajia!

2. Watu na mahitaji yao

*"Pasipo maono,* ***watu huacha kujizuia****; Bali ana heri mtu yule aishikaye sheria."* Mithali 29:18

Maono yatakupa kuwaona watu wakiwa kwenye hali ya uhitaji… watu kwenye hali ya dhambi, mateso, minyororo, uonevu, migandamizo. Hali za namna mbalimbali ambazo ni matokeo ya dhambi na uovu.

Hili neno watu huacha kujizuia ni neno la Kiebrania Pâra' (pau-rah) ambalo laweza kumaanisha vitu kadhaa:

- Kuachilia, kupuuzia, kufungulia, kuacha pekee
- Kukwepa
- Kufunguliwa kutoka kizuizini

Ukiona kundi lolote duniani lipo kwenye "hali dhiki na mashutumu na kuta zao zimebomolewa" (kwa lugha ya Nabii Nabii) basi ujue ya kwamba umeona vyema.

Maono siyo kuona manufaa, faida, matunda yako na namna gani utafaidika kutokea kwa hao watu. Bali ni kwa

namna gai watu hao watanufaika na kufaidika kutoka kwako.

Ukweli ni kwamba watu ni wahitaji kwa kiwango cha kuhurmisha; Yesu alitazama zaidi ya namba, hulka, haiba, mwonekano wa nje - alitazama hitaji la ndani.

*“Na alipowaona makutano, aliwahurumia, kwa sababu walikuwa wamechoka na kutawanyika kama kondoo wasio na mchungaji.”* Mathayo 9:36

*“uwafumbue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuielekea nuru, waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu; kisha wapate msamaha wa dhambi zao, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi.”* Matendo 26:18

Usihadaike na mwonekano wa nje wa watu… tambua ya kwamba watu ni wahitaji. Sisi ni wahitaji. Ndiyo maana Mungu anatafuta mtu ambaye moyo wake utakuwa wazi kudaka viasharia vya mbinguni ili apewe maono. Je, huyo mtu ni wewe?

3. Mahitaji halisi ya kiroho:

Ndiyo, ninakubali watu wana mahitaji mbalimbali. Hata hivyo, ninapendakukazia ya kwamba uhitaji wa kiroho na jawabu lake ndiyo huamua umielele wa watu hao. Kama mwamini, usiishie kuwa na "maono" ya biashara, maduka, siasa… bila kuwa na watu kwenye moyo wa maono hayo. Kama haivuni nafsi, basi haina faida kwenye ufalme.

- Ni wafu katika roho; wanahitaji uhai wa kiroho

*"Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu; hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema."* Efe. 2:1,5

- Wana asili ya dhambi (Zab. 51:5; Efe 2:3) na wanahitaji kugeuzwa 2 Kor 5:17

*"Tazama, mimi naliumbwa katika hali ya uovu; Mama yangu alinichukua mimba hatiani."* Zab:51:5

*"ambao zamani, sisi sote nasi tulienenda kati yao, katika tamaa za miili yetu, tulipoyatimiza mapenzi ya*

*mwili na ya nia, tukawa kwa tabia yetu watoto wa hasira kama na hao wengine."* Efe 2:3

*"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya."* 2 Kor 5:17

- Wako nje ya ufalme wa Mungu na wanahitaji kuzaliwa upya (Yohana 3: 3,5,7)

"Yesu akajibu, akamwambia, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu. Nikodemo akamwambia, Awezaje mtu kuzaliwa, akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa? Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu. Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho. Usistaajabu kwa kuwa nilikuambia, Hamna budi kuzaliwa mara ya pili." Yohana 3:3-7

- Wamepotea kwa nafasi waliyopo (Math 18:11-13)

*"[Kwa maana Mwana wa Adamu alikuja kukiokoa kilichopotea.] Mwaonaje? Mtu akiwa na kondoo mia,*

*mmoja akampotea, je! Hawaachi wale tisa na tisini, akaenda milimani, na kumtafuta yule aliyepotea? Hata akipata kumwona, amin, nawaambia, amfurahia huyo zaidi, kuliko wale tisa na tisini wasiopotea."*

- Wakifa hivi leo wataingia kwenye upotevu wa milele (Yohana 3:36)

*"Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele; asiyemwamini Mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia."* Yohana 3:36

4. Injili na uweza wake

Umewahi kusikia sentensi kama hizi hapo awali:

"Ole wangu!"

"Mimi ni mdogo"

"Mimi siwezi kusema"

"Mimi ni mwanadamu mwenye midomo michafu"

"Mimi ni wa chini kwenye jamaa ya chini ya kabila la chini"

"Mimi simjui mume."

"Sina fedha wala dhahabu"

Ukubwa wa maono utakufanya ujione huna vigezo stahiki. Ni muhimu sana maono yakufikishe hapo. Ukiona maono na ukajiona unatoshea kila nyanja, hujaona maono. Hii hukupelekea kumtaka BWANA. Hukupelekea kuona ngazi ya 3 ya maono. Kuiona injili na uweza wake!

Mfano: Wanafunzi wa Yesu ambao walikuwa watu wa kawaida na/au wa taaluma tofauti (kuna taaluma zilizofahamika ni taaluma za watenda dhambi. Leo useme ndiyo zieneze injili ulimwenguni mwote) ambazo si za kidini kama za wakati huo: Farisayo, Sadukayo, Waalimu, Kuhani, Wazee wa baraza (Hwa ndiyo walikuwa wamesomea dini na kama Yesu angeagiza injili ienezwe basi angechagua makundi ya namna hii ili kuiwezesha na kuipa uhalali )... Wanfunzi wa Yesu hawakuwa na vigezo.

Katika hali ya kulitii agizo kuu alilolitoa BWANA Yesu kwenye kitabu cha injii ya Marko 16:15

Walitii, walienda na walihubiri INJILI tu bila kuwa na mbinu yoyote ile. Kiasi kwamba waliowatazama

waliwaita "... walioupindua ulimwengu." (MDO 17:6) na "wameujaza Yerusalemu yote kwa mafundisho yao." (MDO 5:28)

Injili ni ujumbe wa UWEZA... ni NGUVU inayobadilisha maisha (Rum 1:16; 1 Kor 1:18). Inajitegemea yenyewe!

Ile kwamba injili ina uweza, nguvu na mamlaka inayojitegemea, haimaanishi ya kwamba mhudumu wa injili anapaswa kutojali maswala kama maandalizi na uwasilishaji. Kumtegemea Roho Mtakatifu si kupunguza, kufifisha au kuondoa wajibu wetu wa kimaandalizi.

Neno la Mungu ni toshelevu kuyahudumia maisha ya watu. Mtego mkubwa tulionao sasa ni wa kugeuka na kuwa watoaji wa burudani ili kuendana na zama. Pamoja na mambo mazuri ya kimaandalizi na kiuwasilishaji, neno la Mungu linapaswa kubaki kuwa neno la Mungu. Na hivyo, linaweza kuwavuta watu, kuwageuza watu mioyo na kuleta badiliko la kudumu (Isaya. 55:11)

## 4. **Mimi na wajibu wangu (Isaya 6:8-9)**

Maono yataonyesha kuhusu wajibu wangu, Upande wangu ninaopaswa kuutenda.

i. Mungu anataka nimtumikie
ii. Mungu ana huduma/utumishi na eneo la kiutumishi kwa ajili yangu kwenye shamba lake.
iii. Mungu anataka kunionyesha utumishi na eneo hilo lilipo.
iv. Mungu anataka tumuombe atupe maono, uelewa na mwongozo.

(MDO 26:17)

Paulo (mwebrania wa waebrania) anapewa maono ya kwenda kwa watu wa mataifa [kumbuka Wayahudi na Wasamaria hawachangamani; hawaombani maji ya kunywa; hawakai pamoja]. Si kawaida kabisa. Huyo anaweza kuwa Mungu tu.

MIFANO:

- Ibrahimu: Mwanzo 12:1
- Musa: Kutoka 3:10
- Nehemia: Neh. 1:11
- Paulo: MDO 16:9
- Isaya aliona na kusikia (Isa. 6:1,8)
- Ezekieli aliona na kusikia (Eze. 1:1,28)
- Paulo aliona na kusikia (MDO 16:16,17)

Tunaweza kujua kiasi kuhusu yaliyopita; tunajua kiasi kuhusu yaliyopo LAKINI ni Mungu pekee ajuaye kuhusu yajayo.

Maono yamegungamanishwa na muda (Mh 3:11) – tambua agenda ya maono na muda wa utimilizwaj8 wa maono... Awamu za utekelezaji wa maono (God’s agenda is in phases)

“Musa akasema, Nitageuka sasa, **niyaone maono haya makubwa**, na sababu kijiti hiki hakiteketei.” Kutoka 3:3

Nimemuombea kwa Bwana utaona maono haya makubwa!

Hilo neno maono haya makubwa ni neno linganifu… ikilinganishwa na nini? Musa anasema hivyo kwa kulinganisha na kazi gani nyingine.

Tunajua ya kuwa wakati huo alikuwa anachunga makundi ya mifugo.

Kuna maono makubwa zaidi ya makundi ya kondoo… zaidi ya shughuli hiyo… zaidi ya ajira hiyo… zaidi ya biashara na miradi yako.

Ninakuombea kwa Bwana uone tena kwa jina la Yesu Kristo!

**Kuhusu Mwandishi:**
Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis “Tai”, Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *“Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari.”* [Habakuki 2:14]

**Kuhusu New Vine Church:**
Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

**Mawasiliano na Mwandishi:**



**NEW VINE CHURCH** | **Dodoma**



New Vine Church limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa *(Mathayo 5:13 -14/Yoeli 2:2 - 11).*

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz



**Mahali tulipo:** Swaswa mkabala na geti la Waziri Mkuu, Dodoma mjini.

**Ratiba za Ibada**

**Alhamisi** Saa 11:15 jioni - saa 12:15 jioni

**Jumapili** Saa 3:00 asubuhi - saa 6:30 mchana

nvc_dodoma    +255 754 917 764

# KUHUSU MWANDISHI



James Kalekwa ni amemwamini Yesu kuwa BWANA na Mwokozi wa maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma


pastorjameskalekwa
+255 754 917 764
pastorjameskalekwa
pastorjameskalekwa
pastorjameskalekwa
pastorjameskalekwa
MchungajiJK
+255 754 917 764